# Simbachawene ataka kasi matumizi ya Tehama taasisi za umma nchini

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene amezitaka taasisi za umma ambazo zinasuasua katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kuongeza kasi ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuleta tija katika utendaji kazi wao.

Simbachawene alisema hayo jana wakati wa kufunga Kikao Kazi cha Tano cha Serikali Mtandao kilichofanyika kwa muda wa siku tatu jijini Arusha na kuhudhuriwa na wadau 1,500 wakiwemo maofisa masuuli, wakurugenzi na wakuu wa vitengo vya Tehama, maofisa Tehama na watumiaji wengine wa mifumo ya Tehama kutoka katika taasisi, halmashauri na mashirika mbalimbali ya umma.

Simbachawene alisema serikali imedhamiria kuimarisha na kuongeza matumizi ya Tehama ili kwenda sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa kuwa shughuli nyingi duniani ikiwemo za kiuchumi kwa sasa zinafanyika kwa kutumia Tehama.

Aidha, alisema serikali imetoa kipaumbele kwenye matumizi ya Tehama, hususani katika masuala ya utafiti na ubunifu ili kuimarisha usalama wa mtandao wa mawasiliano na kuongeza watumiaji wa intaneti.

Alisema wizara kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imejipanga kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma mtandao kwa umma kidijiti, sambamba na kuboresha upatikanaji wa mawasiliano ya simu nchi nzima, ili kuwawezesha Watanzania kupata huduma kwa wakati na kwa gharama kupitia mifumo ya Tehama.

"Tunajivunia kuona idadi ya watumiaji wa simu za mkononi pamoja na intaneti, inaongezeka mwaka hadi mwaka. Ongezeko hili linatupa chachu ya kuboresha upatikanaji wa huduma za serikali kupitia simu za mkononi na linadhihirisha ongezeko la matumizi ya Tehama hapa nchini," alisisitiza.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu, Mulula Mahendeka alisema vikao vinavyofanyika vimekuwa na manufaa makubwa katika kukuza na kuendeleza jitihada za Serikali Mtandao, kupitia mawazo mbalimbali yanayotolewa na washiriki wa vikao.

Mahandeka alisema wizara, itasimamia utekelezaji wa maazimio yote yaliyofikiwa kwenye kikao hiki kwa wakati, ikiwa ni kwa wizara yenyewe, e-GA au taasisi nyingine ya umma inayohusika.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Benedict Ndomba alisema mawazo yaliyotolewa ni chachu katika maendeleo ya Serikali Mtandao na mamlaka itayafanyia kazi maoni na mapendekezo yote yaliyotolewa kwa kuwa na jitihada za serikali mtandao zenye tija zaidi.



Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni akizungumza na timu ya wataalamu ya kutoa elimu ya fedha kutoka Wizara ya Fedha na taasisi zake, walipofika ofisini kwake kabla ya kuanza kutoa elimu hiyo kwa wananchi katika Kata ya Stesheni wilayani humo mkoani Kilimanjaro juzi. (Picha na Wizara ya Fedha).

# DC Maswa ashauri Tasaf kurekebisha mfumo miradi ya maendeleo ya jamii

**Na Derick Milton, Maswa**

MKUU wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Aswege Kaminyoge ameshauri kurekebishwa kwa mfumo wa fedha unaotumiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopo chini ya Mpango wa Kunusuru Kaya maskini Awamu ya Tatu (TASAF III).

Kaminyoge alisema mfumo uliopo kwa sasa unasababisha baadhi ya miradi inayotekelezwa katika mpango huo kuchelewa kukamilika kulingana na muda uliopangwa kutokana na taratibu zake kuwa ndefu.

Mkuu huyo wa wilaya alisema hayo juzi mbele ya wajumbe wa Kamati ya kitaifa ya uongozi wa mfuko huo wakati walipotembelea wilaya hiyo kwa ajili ya kukagua miradi mbalimbali ya Tasaf na kuwaona walengwa waliopo kwenye mpango huo.

Alisema mfumo huo wa uletaji fedha za Tasaf kwa ajili ya kutekeleza miradi, unatofautiana na ule mfumo ambao serikali kuu inatumia kuleta fedha serikali za mitaa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kwa mujibu wa Kaminyonge, serikali kuu imekuwa ikipeleka fedha moja kwa moja kwenye kijiji au kata sehemu ambapo mradi wa maendeleo unatekelezwa, hali ambayo imewezesha miradi mingi kukamilika kwa wakati.

Alieleza kuwa kwa utaratibu wa mfumo wa Tasaf, fedha za miradi huletwa kupitia akaunti za halmashauri na kuwa mchakato wa kutoa fedha hizo na kuzipeleka kwenye eneo ambalo mradi unatekelezwa hutumia muda mrefu kukamilika.

"Mfano, mfumo wa fedha za serikali kuu, kama kijiji fulani kinajenga zahanati, fedha huletwa moja kwa moja kwenye hicho kijiji na mradi unatekelezwa kwa haraka na kukamilika," alisema Kaminyonge na kuongeza:

"Lakini mfumo wa Tasaf fedha lazima zitumwe kwenye akauti ya halmashauri, baadaye unafanyika mchakato kutoa hizo fedha kuzipeleka kwenye mradi, hapo ndipo mchakato hutumia muda mrefu na mradi kushindwa kukamilika kwa wakati."

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo wa Wilaya alipongeza uwepo wa mpango wa kunusuru kaya maskini katika wilaya hiyo, kwani umesaidia kwa kiwango kikubwa kaya ambazo zilikuwa maskini kuanza kujitegemea.

Wakizungumza baada ya kutembelea miradi na walengwa, wajumbe wa kamati hiyo walisisitiza zaidi utunzwaji wa miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa na Tasaf ili iweze kudumu kwa muda mrefu na kutoa huduma kwa wananchi wengi.

Walisema kuwa baadhi ya miradi ambayo imetekelezwa na Tasaf katika baadhi ya wilaya, wasimamizi wameshindwa kutimiza majukumu yao kwa kuhakikisha wanaisimamia na kuduma kwa muda mrefu.

"Katika miradi ambayo tunaitekeleza (Tasaf) bado tuna changamoto katika baadhi ya wilaya nchini, usimamizi wake hauridhishi, tunatoa wito miradi hii isimamiwe na itunzwe ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi muda mrefu," alisema mjumbe Richard Shilamba.

# RC Mtwara akabidhi vitanda 20 polisi

**Na Sijawa Omary, Mtwara**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Patrick Sawala amegawa vitanda 20 kwa kikosi cha jeshi la polisi kilichopo Tangazo, Wilaya ya Mtwara.

Alisema hayo wakati akikabidhi vitanda hivyo kwa askari hao na wanajeshi wengine muda mwingi wako kazini hawalali kuhakikisha mkoa huo uko salama, lakini kuna muda wanahitaji kupumzika ili wapate nguvu mpya hivyo vitanda vitawasaidia.

Alivipongeza vyombo hivyo kwa utendaji kazi wao na serikali imeahidi kuendelea kushikamana kama ilivyokuwa kawaida yao ili mkoa na Tanzania kwa ujumla iendelee kuwa mahali salama.

"Kila mmoja mwenye nia njema na anayetamani kuja Mtwara tunamkaribisha ikiwemo kuwekeza, kutalii, kufanya shughuli za kiuchumi na lingine lolote lile kwa sababu vyombo vyetu hivi vinafanya kazi nzuri na wanatoa ushirikiano mkubwa na wanahakikisha mkoa wetu uko salama," alisema Sawala.

Aidha, aliviiomba vyombo hivyo kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa mkoa huo na nchi kwa ujumla ili izidi kuwa salama na amani ambayo imeachwa na waasisi wa nchi hiyo.

Kwa Upande wake, Kamanda wa Jeshi la Polisi, Mkoa wa Mtwara, Issa Suleimani alimshukuru mkuu huyo wa mkoa kwa kutoa msaada huo wa vitanda kwa jeshi hilo.

CamScanner